
MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA





JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

*Na.15. Msimu wa Kilimo 2022/23* *Tathmini ya Februari 11-20, 2023 na Matazamio kwa Kipindi cha Februari 21-28, 2023*

## MUHTASARI

- Mvua zinazotarajiwa katika baadhi ya maeneo nchini zitasaidia katika ukuaji na maendeleo ya mazao
- Kwa ujumla zao la mahindi katika maeneo yanayopata mvua za ***Msimu*** yapo katika hali ya kuridhisha.
- Wakulima, wafugaji na wavuvi wanahimizwa kuzingatia taarifa zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 11-20, 2023


Katika dekadi, mifumo ya migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliimarika wakati ile iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kupungua nguvu. Hali hii iliendelea kuufanya ukanda mvua kuambaa katika maeneo ya kusini mwa nchi.

Joto la bahari katika eneo la mashariki mwa bahari ya Hindi lilikuwa la chini ya wastani wakati upande wa magharibi mwa bahari ya Hindi, joto la bahari lilikuwa la wastani. Hali ambayo haikuwa na mchango katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kutoka katika bahari ya Hindi kuelekea katika maeneo ya pwani ya nchi.

Hata hivyo, upepo katika tabaka la chini ulivuma kutokea magharibi na hivyo kuwa na mchango mkubwa katika kusafirisha upepo wenye unyevunyevu kutokea katika misitu ya Congo kuelekea katika maeneo ya magharibi

## TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 11-20, 2023

Katika dikadi hii maeneo mengi ya nchi yalipata mvua chini ya milimita 10 isipokuwa katika maeneo ya kanda ya kusini na nyanda za juu kusini magharibi ambayo ilipata mvua kati ya milimita 26 na 100. Hata hivyo maeneo machache ya mkoa wa Ruvuma yalipata mvua zaidi ya milimita 100 kama inavyoonekana katika Kielelezo.




Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Februari 11-20, 2023

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 11-20, 2023

Mvua zilizonyesha katika dikadi hii zimeongeza unyevunyevu katika udongo ambao umesaidia ukuaji wa mazao hususan katika maeneo yanayopata mvua za msimu**.**

Kwa ujumla mahindi katika maeneo yanayopata mvua za Msimu yapo katika hali ya kuridhisha, ambapo katika mkoa wa Kigoma na Tabora mahindi yapo katika hata ya kukomaa.

Zao la mpunga lipo katika hatua ya ukuaji katika maeneo ya mikoa ya Tabora, Mbeya, Morogoro na Rukwa, ambapo wakulima wameendelea na palizi.

Katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka hususan Kagera, Shinyanga na Simiyu wakulima wameendelea na shughuli za uvunaji na ukaushaji wa mahindi.

Zao la viazi mviringo lipo katika katika hatua ya kukomaa

katika mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya.

Upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo na wanyamapori umeendelea kuimarika katika maeneo mengi nchini.

## HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 11-20, 2023

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito na mabonde vimeendelea kuongezeka kutokana na mvua zinazoendelea.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 21-28, 2023

Katika dekadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuimarika wakati ile iliyopo kusini mwa dunia ikiimarika kidogo. Hali ambayo inatarajiwa kuendelea kuchochea uwepo wa ukanda mvua (ITCZ) katika baadhi ya maeneo nchini hususani kusini mwa nchi.

Joto la bahari katika eneo la bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la wastani hadi chini ya wastani katika eneo kubwa na hivyo kutokua na mchango katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kutoka katika bahari ya Hindi kuelekea katika maeneo ya pwani ya nchi.

Katika tabaka la chini upepo unatarajiwa kuendelea kuvuma kutokea magharibi hususani katika nusu ya pili ya dekadi, hali inayotarajiwa kuendelea kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kutoka kwenye misitu ya Congo kuelekea nchini hususan meneo ya magharibi mwa nchi.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 21-28, 2023

Maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) na magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) yanatarajiwa kupata vipindi vya mvua na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro) yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) maeneo haya yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache hususan katika nusu ya pili ya dekadi.

Maeneo ya pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) na pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) inatarajiwa kuwa na vipindi vichache vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi hususan katika nusu ya pili ya dekadi.

## HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 21-28, 2023

Mvua zinazotarajiwa hususan katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua zitaongeza unyevunyevu kwenye udongo ambao utasaidia ukuaji na maendeleo ya mazao.

Wakulima hususan wanaopata mvua za Msimu, wanashauriwa kuendelea na shughuli za palizi, uwekaji mbolea, kudhibiti wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea kwa kufuata ushauri wa maafisa ugani wa kilimo.

Wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku, tahadhari, utabiri kwa ajili ya shughuli za baharini na maziwa makuu ili kufanya maamuzi juu ya wakati sahihi wa kwenda kufanya shughuli za uvuvi.

Wakulima, wavuvi na wafugaji wanashauriwa kuzingatia utabiri wa hali ya hewa unaotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.

## HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 21-28, 2023

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kuongezeka kutokana na mvua zinazotarajiwa. Hata hivyo, jamii inashauriwa kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo Kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz; agromet@meteo.go.tz; Tovuti: *www.meteo.go.tz*
(ISO 9001:2015 Certified in Aviation Services)